

MUHTASARI

- Katika kipindi cha Septemba, 1-10, 2017, msimu wa kiangazi uliendelea ijapokuwa mvua za nje ya msimu zilinyesha katika maeneo machache ya mikoa ya Mwanza, Mtwara, Morogoro, Visiwa vya Unguja na Pemba, Kagera, Mara, Shinyanga, Tanga, Kilimanjaro na Dar es Salaam.
- Wakulima wanaopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya msimu wa vuli.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasababisha upungufu wa maji kwa mifugo, hivyo wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na matumizi endelevu ya maji na malisho.
- Vipindi vya upepo mkali vinatarajiwa hususani katika maeneo ya ukanda wa pwani.


**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2017**

Katika kipindi tajwa hapo juu, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo Kusini mwa Dunia (St. Helena na Mascarene) ilianza kudhoofika na hivyo kudhoofisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati ile migandamizo iliyopo Kaskazini ya dunia (Azores na Siberia) ilianza kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa "ITCZ" kushuka kuelekea kusini. Joto la juu kidogo ya Wastani mpaka wastani liliendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati maeneo ya kusini mashariki ya kizio cha kusini mwa Afrika yalikuwa na hali ya ubaridi. Hali hii ilisababisha uwepo wa vipindi vya upepo mkali kutoka kusini na kusini mashariki na hali ya baridi kwenye maeneo ya pwani ya Tanzania.

Kwa upande mwingine joto la bahari la chini ya wastani hadi wastani lilipimwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hii ilipelekea kuwepo na hali ya ukavu kwa maeneo ya magharibi mwa nchi na yale yaliyopo katika ukanda wa ziwa Victoria.

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI
CHA SEPTEMBER 1-10, 2017**

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa tajwa hapo juu, msimu wa kiangazi uliendelea. Hata hivyo, mvua za nje ya msimu wa mvua zilinyesha katika maeneo machache ya mikoa ya Mwanza, Mtwara, Morogoro, Visiwa vya Unguja na Pemba, Kagera, Mara, Shinyanga, Tanga, Kilimanjaro na Dar es Salaam. kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.



Kielelezo 1. Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Septemba 1-10, 2017.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2017**

Wakulima wanaendelea na uandaaji wa mashamba kwa ajili ya mvua za vuli kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua. Pia kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, wakulima wanaendelea na uhifadhi wa mazao na wanajiandaa na msimu ujao wa kilimo.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa mifugo ulikuwa wa wastani katika maeneo mengi ya nchi, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Shinyanga, Singida, Arusha, Manyara na Dodoma ambako hali ya maji na malisho iliendelea kupungua.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 1-10, 2017

Kina na mtiririko wa maji katika mito na mabwawa viliendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu na upepo inayoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo Kusini mwa Dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika na hivyo kudhoofisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati, ile migandamizo iliyopo sehemu za Kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa "ITCZ" kuanza kushuka kuelekea kusini mwa Dunia. Joto la bahari la juu ya wastani hadi wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevu kiasi kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Kwa upande mwingine joto la bahari la chini kidogo ya wastani kwenye maeneo ya kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki linatarajiwa kuendelea. Hali hii inatarajiwa kuendelea kupunguza nguvu ya upepo wenye unyenyevu kutoka katika misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi na kusababisha kuwa makavu.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu) inatarajiwa kuwa makavu na vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo na hali ya ubaridi. **Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara)** yanatarajiwa kuwa makavu na vipindi vichache vya mvua hususani katika maeneo ya miinuko na hali ya ubaridi. **Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba)** yanatarajiwa kuwa makavu ila vipindi vichache vya mvua vinarajiwa hususani katika mkoa wa Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Hali ya baridi na upepo mkali

MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Hali ya ukavu na upepo inayotarajiwa itaathiri upatikanaji wa maji kwa maeneo mengi nchini. Mvua za nje ya msimu zinazotarajiwa hazitoshi kwa uoteshaji wa mazao ya msimu bali zinaweza kuathiri mavuno yasiyohifadhiwa vizuri na mazao ambayo hayajavunwa. Wafugaji wanashauriwa kuchukua hatua stahiki zikiwemo matumizi endelevu ya maji na malisho yaliyopo kwa kuzingatia ushauri kutoka kwa maafisa ugani katika maeneo yao. Pia, wafugaji na wakulima kote nchini wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA SEPTEMBER 11-20, 2017

Kina cha maji katika mabwawa na utiririkaji wa mito vinarajiwa kuendelea kupungua katika maeneo mengi ya nchi kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa. Watumiaji wa maji wanashauriwa kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet1_tz@meteo.go.tz